

## **Upungufu wa Tafsiri ya Lugha ya Ishara katika *Wema Hawajazaliwa* na *Shetani Msalabani***

**Birigitha Ngwano John**  
**Mhadhiri Msaidizi, Chuo cha Uhasibu Arusha**

birigithangwano@gmail.com

### **Ikisiri**

Tafsiri ni miongoni mwa taaluma zinazosaidia kurahisisha mawasiliano miongoni mwa watumiaji wa lugha tofauti. Taaluma hii imekuwa ikinufaisha taaluma nyingine kama vile sheria, utabibu na fasihi. Makala hii inajadili upungufu wa tafsiri ya lugha ya ishara katika *Wema Hawajazaliwa* na *Shetani Msalabani*. Hizi ni riwaya zilizotafsiriwa kwa Kiswahili kutoka katika riwaya ya *The Beautiful Ones are Not Yet Born* na *Devil on the Cross* za Ayi Kwei Armah na Ngugi wa Thiong'o, mtawalia. Aidha, Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano imetumika kama kiunzi cha uchambuzi wa data zilizowasilishwa katika makala hii. Data za makala hii zimepatikana kwa kutumia mbinu ya usaili na uchambuzi wa matini. Makala imebaini kuwa wafasiri wameonesha upungufu katika tafsiri ya lugha ya ishara. Upungufu huo umebainika kupitia vipengele vikuu ambavyo ni upotoshaji, udondoshaji, na tofauti za kiutamaduni. Makala inapendekeza kuwa wafasiri wa kazi za kifasihi wanapaswa kuzingatia misingi ya kiulinganifu katika kutafsiri lugha ya ishara ili kuwafanya wasomaji wao wapate ujumbe uliokusudiwa na waandishi wa matini chanzi.

**Dhana za Msingi:** Upungufu, tafsiri, ishara, lugha ya ishara, fasihi iliyotafsiriwa

## **Utangulizi**

Tafsiri ni zoezi ama mchakato wa uhawilishaji wa mawazo, taarifa na ujumbe wa maandishi kutoka lugha chanzi (LC) kwenda lugha lengwa (LL) (Mwansoko na wenzake, 2006). Hivyo, tunaona kuwa tafsiri siyo tendo tu, bali ni mchakato unaohusisha uchukuaji wa mawazo yaliyo katika maandishi kutoka lugha moja na kuyaweka katika lugha nyingine. Hii ni miongoni mwa taaluma kongwe zilizoanza toka mwanadamu alivyoanza kuwasiliana kwa kutumia lugha. Tafsiri hufanywa katika nyuga mbalimbali kama vile utabibu, sheria na fasihi. Lengo la msingi la tafsiri ni uwezeshaji wa mawasiliano baina ya watu au kikundi cha watu wazungumzao lugha tofauti. Kwa upande wa fasihi, tafsiri imefanyika katika tanzu mbalimbali za fasihi andishi, mathalani nathari, ikijumuisha riwaya, novela na hadithi fupi, tamthiliya, na ushairi. Mekacha (2013) anadokeza kuwa tanzu za nathari na tamthiliya ndizo zimefanyiwa tafsiri kwa idadi kubwa zikilinganishwa na utanzu wa ushairi. Tafsiri ya fasihi ya kigeni imetoa mchango mkubwa katika kupanua fasihi ya Kiswahili. Kwa mfano, kazi za fasihi zilizotafsiriwa kwa Kiswahili ni *Barua Ndefu kama Hii*, iliyotafsiriwa na Clement Maganga; *Wimbo wa Lawino*, iliyotafsiriwa na Paul Sozigwa; *Shetani Msalabani*, iliyotafsiriwa na Ngugi wa Thiong'o; na *Mabepari wa Venisi*, iliyotafsiriwa na Julius Nyerere.

Hata hivyo, zoezi la kutafsiri matini za fasihi si rahisi kwa sababu zimepangiliwa kisanaa. Matatizo ya kufasiri na tafsiri ni ya kimajumui kwa kuwa yamewashughulisha watafiti na wataalamu kote ulimwenguni. Collins (2012) alitafiti kuhusu tafsiri ya fasihi ya wanawake wa Kisenegali. Utafiti wake uliangazia namna wafasiri wa matini za fasihi ya wanawake wanavyofasiri matini hizo kwa kuzingatia hadhira wanayoikusudia ambayo ni wanawake wenyewe. Utafiti wake ulibaini kuwa wafasiri wanabadili na

kuongeza baadhi ya taarifa ambazo hazikuwapo kwenye matini chanzi (MC). Uongezaji na ubadilishaji huo unatokana na ugumu wa kutafsiri matini za kifasihi kwa sababu lugha mbalimbali hutofautiana kutokana na tofauti za kitamaduni katika jamii husika.

Naye Tanjour (2011) anaonesha kuwa tofauti za kitamaduni baina ya lugha ya Kiingereza na Kiarabu ni changamoto katika kufasiri matini za kifasihi. Changamoto hizo zimegawanyika katika makundi makuu mawili ambayo ni: matatizo ya ndani ya isimu na fasihi, na yale ya nje. Matatizo ya ndani ya isimu na fasihi ni kama vile miundo ya sentensi, uteuzi wa maneno, misemo, nahau, methali na tamathali za semi. Matatizo ya nje ya isimu na fasihi huhusisha vyakula, dini, siasa, utawala na usafiri.

Ezika (2012) alichunguza tafsiri ya *Oliver Twist*, akiangazia changamoto na mbinu za tafsiri zikihusisha vipengele vya majina ya wahusika na mandhari. Alibaini matatizo ya tafsiri yanatokana na tofauti za kitamaduni na kimuundo. Suala la uhusika na wahusika, kwa mfano, linaleta changamoto ya kitamaduni, ambapo majina ya wahusika kama vile *Oliver Twist* lilibadilishwa na kuwa *Akabuogu*, likiwa na maana ya “mkono ni pigano” ili liendane na utamaduni wa Ki-Igbo.

Hali kadhalika, katika nchi za Afrika Mashariki, zipo tafiti mbalimbali ambazo zimefanyika kuhusu tafsiri. Mutie (1997) alichunguza changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika kutafsiri matini za kifasihi na kubaini kuwa kuna athari ya kimtindo iliyojitokeza baada ya tafsiri. Naye Ombaga (1986) alibaini kuwa ushairi ni utanzu wa fasihi unaokabiliwa na changamoto nyingi katika kufasiri. Hii ni kwa sababu ushairi ni utanzu

unaosanwa kisanaa kwa kuhusisha lugha ya mkato, arudhi, uwekevu wa maneno na matumizi ya taswira na ishara.

Nchini Tanzania, Malangwa (2005) alibaini kuwa tofauti za kitamaduni ni chanzo kimojawapo cha kutokea kwa matatizo wakati wa kufasiri matini za kifasihi. Hii ni kwa sababu utamaduni hutofautiana kutoka jamii moja na nyingine. Naye Jilala (2014) alichunguza matatizo ya tafsiri katika matini za kitalii nchini Tanzania na kubaini kuwa matatizo hayo yamegawanyika katika makundi makuu matatu ambayo ni matatizo ya kiisimu, matatizo ya kimaana, na matatizo ya kiutamaduni. Aidha, aliona kuwa matatizo haya huleta ukiushi wa ujumbe unaokusudiwa na MC na ule unaofikishwa na matini lengwa (ML); na hii ni kwa sababu lengo la mfasiri hutofautiana na malengo ya mwandishi wa MC.

Lugha ya ishara ni kipengele muhimu katika matumizi ya lugha kwa kuwa waandishi hukitumia katika kujenga maudhui ya kazi husika. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), lugha ya ishara hutokea pale ambapo neno litatumika kuelezea kitu fulani katika kazi ya kifasihi ambacho huwakilisha kitu kingine. Hivyo, ishara ni matumizi ya neno linalobeba dhana, kitu, jambo, hisia, na tukio kuwakilisha kitu kingine. Dhana ya lugha ya ishara na uashiraji imewashughulisha watafiti na wahakiki mbalimbali. Wanyonyi (2015) alichunguza ishara na uashiraji kama nyenzo ya mtindo, maana na kiwakilishi cha itikadi katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*. Alibaini kuwa kuna matumizi ya aina tatu za ishara ambazo ni ishara bia, ishara za kaida na ishara za kifasihi zilizotumika katika riwaya teule ambazo kupitia kwazo alibaini zinawakilisha itikadi.

Pia, Ali (2017) alibaini kuwa matumizi ya lugha yakihusisha matumizi ya semi, tamathali za semi na lugha ya ishara husaidia sana katika kufikisha dhamira kwa wasomaji. Hii ni kwa sababu nyenzo hizo hutumika kama vijenzi muhimu vya kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa wasomaji.

Wataalamu mbalimbali wametafiti kuhusu changamoto za kutafsiri matini za kifasihi, lakini suala la tafsiri ya lugha ya ishara halijashughulikiwa vilivyo. Wafasiri wanapaswa kumakinikia tafsiri ya lugha ya ishara ili ML iwe na mvuto unaokaribia na ule wa MC. Makala hii inalenga kujadili upungufu wa tafsiri ya lugha ya ishara katika riwaya ya *Wema Hawajazaliwa* na *Shetani Msalabani*.

### **Kiunzi cha Nadharia**

Makala hii imetumia Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano kama kiunzi cha uchambuzi wa data. Nadharia hii ni miongoni mwa nadharia tatu zinazolenga kuleta ulinganifu katika tafsiri. Chambilecho Jilala (2016), Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano hulenga kuisitiza mtekenyo sawa wa ujumbe na mtindo baina ya LC na LL. Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano iliasisiwa na Nida (1964) na baadaye iliendelezwa na wataalamu wengine ambao ni Catford (1965), na Nida na Taber (1969).

Pia, nadharia hii imeleta mapinduzi katika tafsiri, hususani kwa kuondoa tofauti zilizokuwapo baina ya utamaduni na isimu. Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano ina mihimili mikuu mitatu. Mosi, suala la usomaji na uelewekaji linasisitiza kuwa MC inapaswa kusomeka na kusikika vema kwa wasomaji kwa namna ya kufikisha taarifa na maudhui pamoja na mtindo. Pili, matini iliyotafsiriwa inapaswa kuzingatia uasilia na ufafanuzi ili iweze kubeba umbo la MC na kumfanya msomaji asome kana kwamba

imeandikwa kwa LL. Tatu, nadharia hii inaweka mkazo katika uzingativu wa athari sawa ambao unahusisha wasomaji wa ML kupata athari sawa kama ilivyo kwa wasomaji wa MC. Katika makala hii, nadharia hii imetumika kujadili upungufu wa tafsiri ya lugha ya ishara katika riwaya ya *Wema Hawajazaliwa* na *Shetani Msalabani*.

### **Methodolojia ya Utafiti**

Makala hii imetokana na utafiti wa kitaamuli uliohusisha mbinu mbili za ukusanyaji wa data ambazo ni uchambuzi wa matini na usaili. Katika uchambuzi wa matini, kulifanyika usomaji wa kina wa MC na ML. Mbinu ya usaili ilihusisha sampuli ya wasailiwa sita ambao ni wanafunzi watatu wa shahada ya uzamivu, na wataalamu watatu wa tafsiri na fasihi katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Matumizi ya mbinu zaidi ya moja ya ukusanyaji wa data yalisaidia upatikanaji wa data halali na thabiti. Makala hii imetumia mkabala wa kitaamuli. Huu ni mkabala ambao hutumia zaidi tafakari katika kuhusisha taarifa mbalimbali za kitafiti na kuhitaji maoni ya kina ya watafitiwa kwa kutumia mbinu ya maelezo (Ponera, 2019). Eneo lililohusika katika ukusanyaji wa data ni Dodoma nchini Tanzania. Eneo hili lilitolewa kutokana na upatikanaji wa maktaba, wanafunzi, na wataalamu wa fasihi na tafsiri kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma.

### **Matokeo ya Utafiti**

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kuna upungufu wa kutafsiri lugha ya ishara katika *Wema Hawajazaliwa* na *Shetani Msalabani*. Upungufu huo umejitokeza katika vipengele vifuatavyo: upungufu unaotokana na upotoshaji, udondoshaji, na tofauti za kiutamaduni. Upungufu unaotokana na upotoshaji umejitokeza katika tafsiri ya dhana ya *Passion Week*. Upungufu unaotokana na udondoshaji umekitwa katika methali na

wahusika na uhusika wa kiishara. Upungufu unaotokana na tofauti za kiutamaduni umejitokeza katika tafsiri ya dhana ya *kenkey*, *latrine* na *circumcision*.

### **Upungufu Unaotokana na Upotoshaji**

Upotoshaji katika tafsiri ni kitendo cha kuwasilisha taarifa zisizo sahihi na tofauti na zile za LC (Lau & Chan, 2004). Kitendo hiki huwafanya wasomaji wa ML wasiweze kuelewa kwa usahihi ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa MC. Katika *Wema Hawajazaliwa*, upungufu wa tafsiri ya lugha ya ishara unaotokana na upotoshaji.

Upotoshaji umejitokeza katika dhana ya *Passion Week*. Utafiti umebaini kuwa dhana ya *Passion Week* iliyoko kwenye MC imepotoshwa katika ML, jambo linaloonesha upungufu katika tafsiri ya lugha ya ishara. Dhana iliyopotoshwa inapatikana katika Sura ya Kwanza ambapo kuna basi, dereva, abiria, na kondakta. Mwandishi anasema:

### **Jozi Na. 1**

**LC:** *Collecting was always easier around Passion Week. Not many passengers needed change; it was enough of a struggle looking round corners and the bottoms of boxes to find small coins somehow overlooked. So, mostly people held out the exact fare and tried not to look into the receiver's face with its knowledge of their impotence. Collecting was certainly easier, but at the same time not as satisfactory as in the swollen days after pay day (uk. 1-2).*

**LL:** Aghalabu ilikuwa ni rahisi kukusanya fedha katika nyakati za mwisho wa wiki kwani si abiria wengi wanaotoa fedha inayohitaji kurudishwa baki. Watu wengi huchukua fedha ya nauli itakiwayo tu. Na wakati wanapoitua hujaribu sana Kutomwangukia usoni yule anayeipokea, kwani uso huo huwa umeshaujua ukosefu wao. Ni kweli ilikuwa si rahisi

kukusanya fedha katika siku kama hizo, lakini hakukuwa kukiridhisha kama katika siku za mishahara (uk. 1 - 2).

Katika data ya Jozi Na. 1, tunaona dhana ya *Passion Week* imedondoshwa katika tafsiri. Tunaona mfasiri ametumia maneno “nyakati za mwisho wa wiki”. Kutokana na tafsiri hii, tumeona kuwa kuna upotoshaji wa dhana ya *Passion Week* ambayo imebeba lugha ya ishara. *Passion Week* ni neno mwambatano lenye maana ya wiki ya mateso na kifo cha Yesu Kristo, kwa mujibu wa imani ya Kikristo. Dhana hii ingeweza kutafsiriwa kama “Wiki ya Mateso” ili kuonesha taabu zinazopatikana katika wiki hiyo. Katika MC, msomaji anaposoma *Passion Week*, anapata lugha ya ishara yenye maana kuwa, katika mwezi, kuna wiki kabla ya siku za mishahara ambayo watu wengi hupitia taabu kutokana na ukosefu wa fedha. Dhana ya *Passion Week* ni lugha ya ishara inayoonesha hali ya umasikini uliopo katika nchi ya Ghana na mataifa mengine yanayoendelea. Wananchi wake wamekuwa na vipato vya chini ambavyo vinatosha tu katika kukidhi mahitaji madogomadogo na kuna kipindi wanakosa fedha na kusubiri mishahara. Pia, upungufu huu wa kutafsiri dhana ya *Passion Week* umejitokeza wakati mwandishi akieleza mazingira ya ofisi. Mwandishi anasema:

## **Jozi Na. 2**

**LC:** *After eight the office began filling up rapidly as the day clerks came in with their little jokes and the talk of bried pay days and perennial Passion Weeks* (uk. 19).

**LL:** Baada ya saa mbili, ofisi ikawa inanza kujaa. Makarani walikuwa wanaingia na dhahaka zao na kuzungumzia siku za mishahara (uk. 20).



Data ya Jozi Na. 2 inaonesha upungufu unaotokana na tafsiri ya dhana ya *Passion Week* ambayo imedondoshwa katika ML. Udondoshwaji huu umeleta athari kwa wasomaji wa ML ambao ni vigumu kuielewa dhana hii kama ilivyo katika MC. Aidha, mwandishi wa MC kuitumia dhana ya *Passion Week* zaidi ya mara moja kunadhihirisha msisitizo wa dhana yenyewe. Kitendo cha mfasiri kupotosha dhana hiyo kinaifanya maana ya kiishara iliyobebwa kupitia dhana ya *Passion Week* isieleweke vyema kwa wasomaji wa ML. Dhana ya *Passion Week* katika MC ni radidi kwa kuwa mwandishi ameipa msisitizo wa kubeba hali ya umaskini unaopatikana kwenye nchi nyingi za ulimwengu wa tatu.

Katika riwaya ya *Wema Hawajazaliwa*, tunaona kuwa mfasiri hakuzingatia urari katika kutafsiri dhana ya *Passion Week*. Urari ni hali ya kuwa na mwendelezo wa neno au dhana kwa namna ileile linapojitokeza mahali tofautitofauti ndani ya kazi moja, hasa ya kifasihi. Kwa mujibu wa Ponera (2019), uandishi mzuri ni ule unaozingatia urari. Utafiti unapendekeza wafasiri wa matini za kifasihi kuzingatia urari, hasa wanapotafsiri dhana zilizobeba lugha ya ishara. Hivyo, tunaweza kusema kuwa ukosefu wa urari husababisha kukosekana kwa mtiririko wa mawazo. Hali hii humfanya msomaji kukosa mvuto anaposoma kazi husika. Katika kutafsiri lugha ya ishara, ni vyema mfasiri kuzingatia urari katika kutafsiri dhana moja inapojitokeza katika mazingira tofauti, lakini ikiwa na maana ileile. Ryanga (1985:168) anasema:

Kama vile ambavyo tungo asilia zisifiwazo kwenye fasihi hutegemea uzuri na ufasaha wa matumizi ya lugha, pamoja na mbinu za kisanaa (siyo maelezo ya kadhia tu), vilevile tafsiri hutegemea mambo hayo. Kama vile ambavyo mtunzi akikosa kuimudu lugha kwa ufasaha

katika sanaa yake wasomaji wake huyaona maandishi yake yakichosha, ndivyo pia ilivyo kwa mfasiri. Wasifu wa tafsiri, kama kazi nyingine za kisanaa, unatokana na utamu wa mdundo wa lugha iliyotumiwa, mfululizo wa taswira na jazanda zikubalikazo katika lugha pokezi, mtiririko wa kadhia na uhifadhi wa ujumbe.

Nukuu hii inasisitiza matumizi sahihi ya lugha ya mfasiri wa kazi ya fasihi. Ryanga (1985) anasisitiza kuwa mfasiri mweledi lazima awe na lugha yenye mdundo, inayoeleweka kinaganaga, aweze kujenga vizuri tungo zake pasi na kuzungukazunguka. Hii inadhihirisha kwamba mfasiri anapaswa kuzingatia urari katika tafsiri yake.

### **Upungufu Unaotokana na Udondoshaji**

Fakih (2018) anafasili udondoshaji kuwa ni kitendo cha kuacha au kuondoa baadhi ya maneno au dhana katika kazi fulani. Kitendo hiki huweza kufanyika kwa kukusudia au bila kukusudia. Stephano na Gwajekera (2019) wanasema kuwa, wakati mwingine, kunaweza kufanyika udondoshaji usio na madhara kutegemeana na elementi zilizoondolewa na utoshelevu wa ujumbe. Katika *Wema Hawajazaliwa*, kuna upungufu wa tafsiri ya lugha ya ishara unaotokana na udondoshaji.

Upungufu wa kutafsiri lugha ya ishara umebainika kupitia udondoshaji wa methali. Aghalabu, methali hufungamanishwa na utamaduni wa jamii fulani kwa kuwa hutumika kutolea mafunzo. Katika riwaya teule, methali ifuatayo imedondoshwa na hivyo kuleta upungufu wa tafsiri ya lugha ya ishara. Mwandishi anasema:

### **Jozi Na. 3**

**LC:** *The driver had not bought it yet, and each of the policemen had said to him in front of everybody, 'Even kola gives pleasure in the chewing' (uk. 95).*

**LL:** Dereva alikuwa bado hajaenda kukata mpya, na kila polisi akamwambia dereva huyo, tena mbele za watu, kwamba atoe rushwa (uk. 102).

Katika data ya Jozi Na. 3, tunaona methali ya “*Even kola gives pleasure in the chewing*” imedondoshwa katika tafsiri. Kwa mujibu wa Mgbemere (2014), kola ni njugu nyekundu inayotokana na tunda la mti wa kola ambao hupandwa sanasana katika eneo la Magharibi la Naijeria. Watu wa Afrika Magharibi huamini kuwa kola hubeba bahati nzuri au mbaya. Bahati hii huhusishwa na idadi ya vipande vya njugu zinazopatikana ndani yake. Mtu anayeivunja kola hiyo huweza kuathiri watu wengine. Methali hii imebeba lugha ya ishara yenye maana kuwa suala la rushwa ni la kawaida tu katika nchi ya Ghana. Kola inafananishwa na kitendo cha rushwa ambacho kinaleta furaha kwa mtafunaji.

Hivyo, imebainika kuwa udondoshaji huo uliofanyika kwenye data ya Jozi Na. 3 ungeweza kuepokwa kwa mfasiri kutumia methali linganifu ya LL kama “Nifae kwa jua, nikufae kwa mvua”. Mfasiri alipaswa kufahamu utamaduni wa LC, ambao ni utamaduni wa watu wa Afrika Magharibi. Kama tulivyokwishaona, kola ni aina ya njugu ambayo ni nyekundu inayoliwa kama sehemu ya utamaduni wa makabila mbalimbali yanayopatikana Afrika Magharibi, kama vile Waakan nchini Ghana, na Waigbo nchini Naijeria. Abbas (2015) anasema kuwa wafasiri wa matini za kifasihi wanapaswa kupata visawe vyenye ulinganifu unaokaribiana kimaana na visawe vya LC. Mawazo haya yanasisitiza msingi wa Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano unaohusu kuwapo kwa athari sawa katika tafsiri. Hivyo, katika data ya Jozi Na. 3, mfasiri angeweza kutafuta kisawe

kinachokaribiana na kola, kisha kutafsiri msemu ili ueleweke kwa wasomaji wa LL.

Pia, katika riwaya ya *Shetani Msalabani*, udondoshaji unajidhihirisha katika majina ya wahusika. Utafiti umebaini kuwa kuna baadhi ya wahusika wenye kubeba lugha ya ishara katika MC ambao wamedondoshwa katika ML. Tunaona mhusika Kamoongonye amedondoshwa, na; badala yake, mwandishi ametumia jina lingine ambalo ni Mchumba kijana. Huyu ni mhusika mwingine ambaye ametumika kiishara katika riwaya hii. Mhusika huyu ametumika pale ambapo inahadithiwa hadithi ya Kaledi kama ifuatavyo:

#### **Jozi Na. 4**

**LC:** *Before a month is up, Kareendi finds herself a Kamoongonye. The young man is a university student (uk. 20).*

**LL:** Kabla ya mwezi kwisha, Kaledi amejipatia Mchumba kijana. Ni mwanafunzi wa chuo kikuu (uk. 18).

Kupitia data ya Jozi Na. 4, tunaona mhusika Kamoongonye akitafsiriwa kuwa “Mchumba kijana”. Mfasiri ameliacha jina la Kamoongonye ambalo limebeba lugha ya ishara na limefafanuliwa vizuri katika MC. Mwandishi, kupitia tiniwayo, ameeleza kuwa Kamoongonye ni mhusika wa ngano ya Wakikuyu inayohusu msichana mdogo anayelazimishwa na baba yake kuolewa na Waigoko ambaye ni mzee tajiri. Msichana huyo anakataa kuolewa na mzee huyo kwa kuwa ana mchumba wake masikini anayelitwa Kamoongonye. Katika MC, tunaona mhusika Kamoongonye amebeba lugha ya ishara yenye maana mbalimbali. Mosi, Kamoongonye anamwakilisha mhusika mwingine anayelitwa John Kimwana ambaye alikuwa mchumba

wa Wariinga. John Kimwana ni kijana mwenye hali duni ya kiuchumi. Pili, Kamoongonye anawakilisha vijana wengine ambao ni maskini kiasi cha kudharauliwa na kukataliwa katika jamii hususani wakati wa kutaka kuoa. Maelezo ya uhusika wa Kamoongonye yamedondoshwa katika ML na kumfanya msomaji wa ML ashindwe kupata ufafanuzi mzuri kuhusu lugha ya ishara inayomaanishwa kupitia mhusika Kamoongonye.

Pia, kuna mhusika Waigoko ambaye amedondoshwa katika tafsiri. Hii inaonekana wakati mwandishi anasimulia hadithi ya Kaledi. Anasema:

### **Jozi Na. 5**

**LC:** *He declares that he knows very well that Kareendi has rumped Waigoko Kihara's bed, that Kihara is not even the first to eat from Kareendi's things, that a girl who has sipped at the delights of money can never stop drinking (uk. 25).*

**LL:** Anasema anajua bayana kuwa Kaledi anakijua nje ndani kitanda cha Boss Kihara. Hata huyo Boss wake si wa kwanza aliyecheza ngoma mapajani mwa Kaledi. Ati msichana aliyeonja pesa na furaha inayoandamana nazo hawezi kukataa kwa urahisi (uk. 25).

Data ya Jozi Na. 5 inaonesha udondoshaji wa jina “Waigoko” ambalo limetumika kama lugha ya ishara kwenye MC. Jina hili limefafanuliwa vyema na mwandishi kuwa Waigoko ni mhusika tajiri anayepatikana katika ngano ya Wakikuyu. Katika hadithi hii, tunaona kuna baba mmoja akimlazimisha mtoto wake aolewe na bwana mmoja tajiri aitwaye Waigoko. Hii inaonesha kuwa Waigoko ni mhusika wa kiishara ambaye ametumika kuwakilisha wakina baba watu wazima ambao ni matajiri, na

wanatumia utajiri wao kuwalaghai mabinti na kuwa nao katika mahusiano, lakini, mwishoni, huwatelekeza na kutafuta mabinti wengine.

Mfasiri wa matini za kifasihi anapaswa afahamu mikakati mbalimbali ya kiuandishi inayomsaidia kutafsiri lugha ya ishara. Katika data ya Jozi Na. 4 na data ya Jozi. Na. 5, mikakati ambayo ingeweza kutumika ni pamoja na matumizi ya mbinu ya ufafanuzi inayohusisha matumizi ya tiniwayo na faharasa. Pembe (2016) anasema kuwa mbinu ya ufafanuzi katika tafsiri husaidia kueleza kitu au jambo waziwazi ili kusaidia hadhira lengwa kulielewa. Mbinu hii inafaa zaidi katika kuhawilisha masuala yanayofungamanishwa na utamaduni wa LC. Njia hii humpa mfasiri uhuru wa kuongeza ufafanuzi wa kipengele fulani kinachowakilisha lugha ya ishara. Lengo la kufafanua kipengele hicho ni kumfanya msomaji wa LL apate athari sawa ya kisanaa kama ilivyo katika msomaji wa LC. Nida (1964) anadokeza kuwa suala muhimu katika zoezi la tafsiri ni kuzingatia maana na ujumbe wa kile kinachoelezwa kwa lugha nyingine kiweze kuwafikia watu wengine kwa kutumia lugha tofauti. Hivyo, kwa kuzingatia Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano, zoezi la tafsiri hususisha uhawilishaji wa mawazo pasipo kupoteza maana msingi kati ya LC na LL.

Pia, mbinu ya ufafanuzi hutumika zaidi hasa pale lugha ya ishara katika LC inapokuwa na maana pana na huenda maelezo yake yakamchanganya msomaji. Nzyoka (2014) anasema kuwa, kuna wakati mfasiri asipotumia mbinu ya ufafanuzi, anasababisha maana ya kiishara kufinywa. Hivyo, tunaona kuwa ufafanuzi unasaidia kuondoa utata kwa wasomaji. Mbinu ya ufafanuzi ni muhimu katika kutafsiri majina ya wahusika yaliyotumika katika MC na yana maana fulani katika utamaduni wa jamii ya LC. Hii

inafanyika ili kutopoteza maana ya MC katika ML. Mbinu hii ya ufafanuzi hufanikishwa kwa kutumia namna zifuatazo:

Mosi, mbinu ya ufafanuzi hufanikishwa kupitia matumizi ya tiniwayo. Tiniwayo ni maelezo ya ziada kuhusu neno au dhana fulani yanayowekwa chini ya ukurasa. Maelezo haya yanalenga kutoa ufafanuzi ili kumsaidia msomaji kuelewa vizuri neno au dhana tajwa katika ukusara husika. Ponera (2019) anasema kuwa neno au kipande cha matini kinachopaswa kufafanuliwa huwekwa namba mbele - juu yake. Mbinu hii ni muhimu katika kutafsiri lugha ya ishara kwa sababu humsaidia mfasiri kutoa maelezo kwa baadhi ya dhana zinazobeba lugha ya ishara ambazo anahisi msomaji wa ML anaweza asizielewe vizuri.

Kwa mfano, katika data ya Jozi. Na. 4, mfasiri ameonesha upungufu wa tafsiri ya lugha ya ishara, hususani, pale anapoacha kutumia tiniwayo kwa baadhi ya maneno kama Kamaongonye yaliyobeba lugha ya ishara ambayo yamefafanuliwa kwa kutumia tiniwayo katika MC. Kwenye MC, mwandishi ametumia tiniwayo kueleza kuhusu Kamaongonye ambaye ni mhusika anayebeba lugha ya ishara. Mwandishi anasema:

*\*Kamaongonye is a character in Gikuyu ballad about a young girl whose father wants her to marry Waigoko, a rich old man with a hairy chest, while she prefers her own choice, a poor young man, Kamaongonye (uk. 20).*

Mfano wa tiniwayo hapo haukuwekwa katika ML. Tunaona kuwa tiniwayo hiyo imemsaidia msomaji wa MC kuelewa mhusika wa kiishara Kamaongonye aliyepo kwenye hadithi ya Wakikuyu inayomhusu msichana

mdogo kulazimishwa kuolewa na Waigoko kinyume na matwaka yake kwa kuwa ana mchumba wake Kamoongonye.

Mbinu ya pili inayotumiwa ili kufanikisha ufafanuzi ni matumizi ya faharasa. Faharasa huwa na sifa mbalimbali. Mosi, faharasa ni orodha ya maneno ambayo hupangwa kwa alfabeti, kuanzia maneno yanayoanza na alfabeti A hadi Z. Lengo la kupanga kialfabeti ni kumrahisishia msomaji kazi ya kutafuta neno husika wakati wa usomaji wa matini. Bakize (2020) anasema kuwa, ikiwa faharasa hazijapangiliwa vizuri, kuna uwezekano majina, mada na maneno yanayooneshwa kwenye faharasa yakapishana na ya kwenye kurasa halisi kitabuni. Hii inadhihirisha kuwa mfasiri anapaswa kuwa makini katika uandishi wa faharasa. Pili, faharasa hufafanua maneno magumu au yasiyoeleweka kwa urahisi kwa wasomaji wa matini husika (Mdee, 1998). Hivyo, tunaweza kusema kuwa si kila neno linakidhi haja ya kuwekwa kwenye orodha ya faharasa. Tatu, faharasa huwekwa mwishoni mwa matini ili kumsaidia msomaji kuelewa baadhi ya dhana ambazo hazikufafanuliwa vizuri ndani ya kitabu. Bakize (khj) anasema kuwa faharasa ni kama kipengele cha yaliyomo kilichopanuliwa zaidi. Nne, faharasa huambatana na matumizi ya kurasa ambazo maneno hayo yanapatikana ndani ya matini. Matumizi ya kurasa humsaidia msomaji kufanya urejeleaji wa maneno husika.

Kwa mujibu wa Mdee (2020), faharasa ni mbinu iliyoanza kutumika muda mrefu huko Ugiriki katika karne ya tano kabla ya kuzaliwa Kristo. Katika utanzu wa ushairi, faharasa hutumika sana. Tunaona washairi kama vile Shaaban Robert, Amri Abeid Kalutta, Saadan Kandoro, Mathias Mnyampala na Mohamed Seif Khatib wametumia faharasa katika diwani zao. Faharasa hujulikana kama kamusi ndogo (Abedi, 1954). Kwa mujibu



wa Hassan (2022), kutumia faharasa katika taaluma ya uandishi na tafsiri kuna umuhimu ufuatao: Mosi, faharasa husaidia kukuza taaluma ya Leksikografia. Maneno magumu yanayofafanuliwa katika faharasa huwapa nafasi watunzi wa kamusi kupata vitomeo vya kuingiza katika kamusi. Pili, faharasa husaidia kuhifadhi misamiati ya lugha. Maneno yanayofafanuliwa katika faharasa huweza kutumika kwa vizazi vijavyo. Tatu, faharasa husaidia kumpa uelewa msomaji wa kazi husika. Msomaji anapokutana na ufafanuzi wa neno katika faharasa, huelewa na kupata ujumbe kwa namna iliyokusudiwa na mwandishi.

Utafiti umebaini kuwa wafasiri wa kazi za kifasihi wanaweza kutumia mbinu hii kuelezea baadhi ya dhana zinazobeba lugha ya ishara. Kwa mfano, katika Jozi Na. 4, mfasiri angeweza kutumia faharasa na wasomaji wakaelewa vizuri ujumbe uliokusudiwa. Kamoongonye ametafsiriwa kuwa mchumba kijana, kitu kinachopausha maana ya kiishara inayopatikana kupitia jina la Kamoongonye. Maana hii inajitokeza vizuri katika MC. Faharasa ingefaa kutumika kwa kuwa msomaji wa ML angeelewa vizuri maana inayopatikana katika jina Kamoongonye. Kupitia faharasa, mfasiri angeweza kutoa ufafanuzi kuwa kuhusu mhusika Kamoongonye kiasi cha kumfanya msomaji wa ML kupata ujumbe uliokusudiwa.

Aidha, matumizi ya faharasa yanafaa katika kutafsiri dhana ya Waigoko inayojitokeza kwenye data ya Jozi Na. 5. Tunaona mfasiri amedondosha dhana ya “Waigoko” ambayo angeweza kuitolea ufafanuzi kupitia faharasa na wasomaji wakaelewa. Dhana hii ni lugha ya ishara inayobeba maana ya watu wazima ambao ni matajiri wanaowatumia wanawake kama vyombo vya starehe ilihali wana wake zao wa ndoa. Malima (2018) anasema kuwa

watu wenye tabia hizi hujulikana kama “fataki”. Neno hili ni neno la msimu linalotumika kurejelea mwanaume mwenye wapenzi wengi.

### **Upungufu Unaotokana na Tofauti za Kiutamaduni**

Upungufu mwingine unaojitokeza katika tafsiri ya lugha ya ishara ni ule unaotokana na tofauti za kiutamaduni baina ya LC na LL. John (2018) anafasili utamaduni kuwa ni utaratibu uliowekwa na binadamu katika kuyakabili maisha yake ya kila siku. Utaratibu huu hutumika kama kigezo cha kutofautisha jamii moja na nyingine. Utamaduni huhusisha vipengele mbalimbali kama vile mila, desturi, mifumo milo (vyakula na vinywaji), sanaa za maonesho, na lugha. Wanjala (2011) anasema kwamba wafasiri hupata ugumu wa kutafsiri matini za kifasihi kutokana na tofauti za kiutamaduni baina ya lugha mbalimbali. Katika maelezo haya, tunaona upungufu uliojitokeza unapausha lugha ya ishara. Hii ni kwa sababu utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wa mambo na taratibu za kuendesha maisha zinazowatofautisha watu wa jamii moja na nyingine. Kila jamii ina utamaduni wake. Hivyo, utamaduni fulani unaweza kuwa mzuri kwa jamii moja, lakini ukawa mbaya kwa jamii nyingine. Ufuatao ni upungufu uliobainika katika riwaya ya *Wema Hawajazaliwa*:

Upungufu wa kwanza unaojitokeza katika riwaya hii ni tafsiri ya dhana ya *Kenkey*. Ni ukweli usiopingika kuwa wafasiri wa matini za kifasihi huwiwa vigumu kupata visawe vyenye mwegamo wa kiutamaduni katika LL. Kwa kuzingatia mhimili wa Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano, mfasiri anaweza kutafuta visawe vyenye maana inayokaribiana au inayolingana katika LL kwa lengo la kuleta athari sawa ya kimaana na visawe vilivyotumika katika LC. Utafiti umebaini kuwa dhana ya *Kenkey* imeachwa jinsi ilivyo bila kutolewa maelezo au ufafanuzi wowote, jambo linalomfanya msomaji wa ML kutoelewa kikamilifu ujumbe uliokusudiwa.

Hii inaonekana pale Yule bwana anapoelekea ofisini, na, akiwa njiani, anaona mambo kadhaa. Mwandishi anasema:

### Jozi Na. 6

**LC:** *People still used them, and they overflowed with banana peels and mango seeds and thoroughly sucked-out oranges and the chaff of sugarcane and most of all the thick Brown wrapping from a hundred balls of Kenkey* (uk. 8).

**LL:** Na bado watu wakawa wanaendelea kuvitumia. Vikajaa kupita kiasi. Vikajaa maganda ya ndizi, kokwa za maembe, makaka ya machungwa, matapu ya miwa, na karatasi za rangi ya kahawia ambazo hufungia Kenkey (uk. 8).

Katika data ya Jozi Na. 6, tunaona mfasiri ameacha neno *Kenkey* kama lilivyo kwenye MC. Hapo, tunaona kifungu cha maneno “*Brown wrapping from a hundred balls of Kenkey*” kimetafsiriwa kuwa “karatasi za rangi ya kahawia ambazo hufungia *Kenkey*”. Tukisoma MC, tutaona kuwa, katika sehemu hiyo, kulikuwa na karatasi nyingi za kufungia vifungashio vya mviringo mia moja vya *Kenkey*. Kwa mujibu wa Adom (2018), *Kenkey* ni chakula kinacholiwa zaidi Afrika Magharibi, hususani, katika nchi ya Ghana. Chakula hiki kinatengenezwa kwa mahindi meupe na huliwa na samaki, hasa waliokaangwa. Aghalabu, chakula hiki kinaliwa katika koo za kichifu. Katika MC, msomaji anaona namna chakula hiki kinavyoliwa kwa wingi na ndiyo maana tunaona kuna karatasi nyingi zilizotumika kufungashia *Kenkey* kwenye umbo la mviringo. Utafiti umebaini kuwa mfasiri hakuonesha bayana idadi hiyo ya vifungashio vya *Kenkey* ambayo ilikuwa inaashiria uchafu unaofanywa na viongozi kwa kuwakilishwa na uchafu unaotoka kwenye vyombo vya kuwekea taka. Pia, mfasiri hakufafanua kuhusu chakula hiki, kitu kinachomwia vigumu msomaji kuelewa dhana inayozungumziwa. Hivyo, mfasiri alipaswa kuufahamu

vyema utamaduni wa watu wa Ghana ambao ndio hasa hadhira lengwa na kuufahamu utamaduni wa hadhira anayoikusudia ili atafute kisawe chenye ulinganifu unaokaribiana na ule wa kisawe cha LC.

Pili, dhana ya *latrine* imetafsiriwa kwa namna inayoleta upungufu unaotokana na tofauti za kiutamaduni. Hii inajitokeza wakati Koomson anamwambia Yule bwana ampeleke chooni kwa sababu alikuwa amebanwa na haja, ndipo Oyo, ambaye ni mke wa Yule bwana, anajibu:

### **Jozi Na. 7**

**LC:** *“We don’t have a toilet here.” Oyo looked astonished. Preening herself, Estella asked, ‘So how do you er... what do you do?’ The man, enjoying himself now, gave her a long reply. ‘We have a place all right,’ he said, ‘only it isn’t anything high class. It isn’t a toilet, you see. Just a latrine’* (uk. 133-134).

**LL:** “Hatuna choo hapa,” Oyo akaonyesha kushangaa. Estella akauliza, “Kwa hiyo ninyi hu... hufanyaje? Yule bwana, huku anaona raha, akampa Estella kipande cha jawabu. “Choo kipo,” akasema, lakini si cha kwendewa na watu wakubwa. Si choo kamili. Ni cha kunyia tu” (uk. 144).

Katika data ya Jozi Na. 7, tunaona kuwa Oyo anasema kuwa wao hawana choo kwa sababu kilichopo si kizuri na ndiyo maana hapendelei kukiita choo badala yake anasema kuwa hicho ni cha kunyia tu. Kifungu cha maneno *“Just a latrine”* kimetafsiriwa kuwa “Ni cha kunyia tu”. Tafsihi hii ina upungufu katika lugha ya ishara. Dhana ya *latrine* kwa muktadha wa mazingira ya kiutumizi ingepaswa kutafsiriwa kuwa “choo cha shimo”. Kitendo cha mfasiri kutumia maneno “Ni cha kunyia tu” badala ya “choo cha shimo” kimeleta upungufu uliokitwa katika masuala ya kitamaduni. Kiafrika, choo cha shimo ni sehemu ya nyumba au mahali ambapo watu

huenda kujisaidia na kuoga. Dhana hii ya *latrine* katika MC imebeba lugha ya ishara inayomaanisha hali duni ya makazi iliyopo kwenye nyumba ya Yule bwana. Stephano (2016) anasema kuwa wafasiri wa matini za kifasihi ni vyema kuzifahamu tamaduni za jamii ya LC na LL. Hii ni kwa sababu matini za kifasihi hubeba dhana nyingi za kitamaduni. Hivyo basi, ili lugha ya ishara itafsiriwe kwa ufanisi, ni vyema kwa wafasiri kufahamu vyema utamaduni wa LC na LL. Hii itasaidia katika kumakinikia baadhi ya dhana zilizobeba lugha ya ishara na zilizokitwa katika masuala ya kitamaduni.

Pia, mfasiri kutotafsiri sawasawa dhana ya *latrine* katika data ya Jozi Na. 7 kunafanya ujumbe kusudiwa kutofika ipasavyo kwa wasomaji wa ML. Hapa, tunaona mfasiri hakuzingatia utamaduni wa LL kwa sababu, katika lugha ya Kiswahili, kuna baadhi ya maneno ambayo hutamkwa kwa kutumia tafsida. Kitendo cha mfasiri kusema “Ni cha kunyia tu” kinaonesha kutozingatia utamaduni wa Waswahili ambao hutumia tafsida kama vile “hutumika kujisaidia”. Pia, mfasiri hakuzingatia utamaduni wa hadhira lengwa katika kutafsiri lugha ya ishara iliyokitwa kwenye dhana za kitamaduni kupitia neno *latrine*.

Pia, katika riwaya ya *Shetani Msalabani* kumbainika upungufu kadhaa unaotokana na tofauti za kiutamaduni. Mosi, kupitia majibizano kati ya Boss Kihara na Kaledi.

### **Jozi Na. 8**

**LC:** *What are you afraid of? What is the problem? “I have a Kamoongonye, a young lover.” “Ha! Kareendi, don’t make me laugh. Are you really so old-fashioned? Are you talking about one of those boys who pretend to be men? Those boys, are they even circumcised?” (uk. 22)*

**LL:** Waogopa nini? Ni yapi unayoyahofia? “Nina mchumba wangu kijana!” “Ha ha ha ha! Usinichekeshe Kaledi. Umekuwa oldfashioned? yaani hawa vijana waliozaliwa juzi? Vijana wanaojikweza kujaribu kujitia katika tabaka za wanaume. Wana nini hawa? Maskini wa kupindukia! Hawa ni wa kuhurumia tu! (uk. 22)

Katika data ya Jozi Na. 8, kifungu cha maneno “*Those boys, are they even circumcised?*” kimetafsiriwa kuwa “Wana nini hawa? Maskini wa kupindukia! Hawa ni wa kuwahurumia”. Tunaona kuna upotoshwaji wa tafsiri, jambo linaloibua upungufu katika lugha ya ishara. Jambo linalosisitizwa na mwandishi wa MC ni kitendo cha vijana kutotahiriwa, ambacho kinabeba lugha ya ishara. Mfasiri angeweza kutafsiri kwa kutumia kifungu cha maneno “Wavulana hao wametahiriwa kweli?” Katika utamaduni wa jamii nyingi za Kiafrika, kitendo cha mwanaume kutahiriwa kinabeba ushababi wa mwanaume. Jamii huwaona ambao hawakutahiriwa kuwa hawajakamilika na kuonekana kuwa kama watoto. Boss Kihara anatumia maneno hayo kumwambia Kaledi kuwa vijana wengine waliozaliwa juzi hawajatahiriwa.

### **Hitimisho**

Makala hii imejadili upungufu wa tafsiri ya lugha ya ishara kwa kujikita katika riwaya ya *Wema Hawajazaliwa* na *Shetani Msalabani*. Imebainika kuwa baadhi ya wafasiri wa matini za kifasihi wana upungufu katika kutafsiri baadhi ya dhana zinazobeba lugha ya ishara. Kupitia upungufu uliobainishwa, wasomaji wa ML wanakosa ujumbe uliokosudiwa kulinganisha na wasomaji wa MC. Hivyo basi, makala inapendekeza wafasiri wa matini za kifasihi kuzingatia Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano katika tafsiri. Hali hii itasaidia wasomaji wa ML kupata

ujumbe kupitia lugha ya ishara wenye mtekenyo sawa kiulinganifu na ule waupatao wasomaji wa MC.

### **Marejeleo**

- Abbas, F. (2015). An Analysis of Translation Methods for English Proverbs: Literal, Literary or Substitution. *European Academic Research*, II, 14016 - 14026.
- Abedi, K. A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: East African Bureau.
- Adom, D. (2018). The Impacts of Culture in Food Preferences in Ghana, in Paul, P. K. (Eds.). *Trends and Prospects in Food Technology, Processing and Preservation*. New Delhi: Today and Tomorrow's Printers & Publishers.
- Ali, S. K. (2017). Kuchunguza Matumizi ya Lugha na Dhamira katika Tamthilia Teule za Mwandishi Emmanuel Mbogo, (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- BAKITA. (2016). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.
- Bakize, L. (2020). *Mbinu na Mikakati ya Uandishi na Uchapishaji*. Dar es Salaam: Eternal Word and Charity Publishing (EWCP).
- Catford, J. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*. London: Oxford University Press.
- Collins, G. (2012) Gendering Translation: the 'Female Voice' in Postcolonial Senegal. *Francosphères*, 1 (2),127-147.
- Ezika, C. G. (2012). A Translation of Oliver Twist by Charles Dickens: Problems and Principles (Unpublished Master's Dissertation), University of Nigeria.

- Fakih, A. H. (2018). Changamoto za kutafsiri riwaya: Mifano kutoka tafsiri ya Kiswahili ya riwaya ya Robinson Crusoe (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Jilala, H. (2014). Athari za Kitamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka Matini za Kitalii katika Makumbusho za Tanzania (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa), University of Dar es Salaam.
- Jilala, H. (2016). Uchambuzi wa Nadharia ya Ulinganifu katika Fasihi, katika Jilala, H. (Mh.). *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Undaji wa Istilahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Limited.
- John, B. N. (2018). Usawiri wa Utamaduni wa Hadhira Lengwa katika Riwaya Zilizotafsiriwa kwa Kiswahili: Mifano kutoka Barua Ndefu kama Hii (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Hassan, H. R. (2022). Faharasa katika Diwani za Said Ahmed Mohamed: Vijenzi na Tija Zake. *Jarida la CHAKAMA*. 1, 53 - 60.
- Kihore, Y. M. (2005). Uzingativu wa Sarufi katika Tafsiri. *Swahili Forum*, 12, 109 - 120.
- Malangwa, P. (2005). Problems of Translating Literary Works: The Case of Julius Kambarage Nyerere's Translation of the Play *Mabepari wa Venisi* (Unpublished Master's Dissertation), University of Dar es Salaam.
- Malima, C. C. (2018). Kuchunguza Matumizi ya Misimu ya Wanavyuo Inavyotumika katika Mitandao ya Kijamii Mjini Morogoro (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mdee, J. S. (1998). Faharasa za Shaaban Robert na Mchango wake katika Leksikografia ya Kiswahili. *Mulika*, 24, 14 - 31.
- Mekacha, R. D. K. (2013). Tafsiri ya Ushairi, katika Mwansoko, H.J.M, Mekacha, R.D.K, Masoko, D. L.W na Mtesigwa, P. C. L. *Kitangulizi cha Fasihi. Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.



- Mgbemere, C. D. (2014). Cues in Igbo Cultural Making Matrix: Analysis of Achebe's *Arrow of God*. *Journal of Culture, Society and Development*, 4, 19 - 26.
- Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mshindo, B. H. (2010). *Kufasili na Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Zanzibar: Chuo Kikuu cha Chukwani.
- Mutie, E. (1997). *Sanaa katika Tafsiri: Matatizo na Athari zake* (Tasinifu ya ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mwansoko, H. J. M., Mekacha, R.D.K, Masoko, D. L.W na Mtesigwa, P. C. L. (2013). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Nida, E. (1964). *Toward a Science of Translation*. Leiden: E. J. Brill.
- Nida, E. & Taber, C. R. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Shanghai: Foreign Language Education Press.
- Nzyoka, S. (2014). Tathmini ya Tafsiri na Mikakati ya Kutafsiri Tamathali za Usemi katika Tamthilia ya Antigoni (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Ombaga, Z. (1986). Fasihi: Tafsiri katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili Matatizo na Athari Zake (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Pembe, H. (2016). Tafsiri ya Mazungumzo katika Filamu za Kiswahili. *Huria Journal of the Open University of Tanzania*, 21.
- Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.
- Ryanga, S. C. W. A. (1985). Vitabu vya Kutafsiriwa na Fasihi ya Kiswahili. *Jarida la TUKI*, 162-175.

- Stephano, R. (2016). *Nadharia ya Mifumo Mingi: Suluhisho la Matatizo ya Tafsiri za Kifasihi*, katika Jilala, H. (Mh.). *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Limited.
- Stephano, R. & Gwajekera, F. D. (2019). Ufanisi wa Tafsiri za Viwandani Nchini Tanzania: Uchunguzi wa Vifungashio vya Dawa za Binadamu. *Mulika*, 38, 26 - 42.
- Tanjour, M. (2011). *Bridging Cultural Gaps in English- Arabic Translation* (Unpublished PhD Thesis), The University of Leeds.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Limited.
- Wanjala, S. F. (2011). *Misingi ya Ukalimani na Tafsiri*. Mwanza: Serengeti Educational Publisher (T) Limited.